

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

SHULE YA SEKONDARI NGUDU,
S. L. P 49,
NGUDU KWIMBA.
TAREHE

NGSS/FV.J.INS/VOL1/2016

MZAZI/MLEZI WA

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2016**

1. Ninayo furaha kukufahamisha kuwa
mwanao

AMECHAGULIWA kujiunga na masomo ya **KIDATO CHA TANO** MCHEPUO WA
katika **SHULE YA SEKONDARI NGUDU. HONGERA SANA.** Shule itafunguliwa tarehe 11/07/2016.

2. Shule hii ni ya kutwa na mchanganyiko kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne na ya bweni kwa wavulana **kidato cha tano na sita.**
3. Kwa kuwa mwanao ni mmoja wa wachache waliobahatika kuchaguliwa kuanza masomo ya sekondari kidato cha tano, natumaini utamsisitiza kutumia vizuri nafasi hii aliyopewa kwa kusoma kwa bidii na kwa nidhamu ya hali ya juu ili kufanya vizuri kitaaluma.
4. **MAHALI ILIPO:** Shule iko **Ngudu Mjini** makao makuu ya Wilaya ya **Kwimba** mkoani **Mwanza.**
Kwa wale wanaotoka nje ya mkoa wa Mwanza, unashauriwa kusafiri hadi Jijini Mwanza na kushuka stendi kuu ya mkoa ya **Nyegezi.** Hapo utakuta mabasi madogomadogo yatakayokupeleka hadi Ngudu Mjini. Shule iko umbali wa **KM 0.5** kutoka stendi ya Ngudu Mjini karibu na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kwimba.

TUNAKUTAKIA SAFARI NJEMA

A. SARE YA SHULE (DARASANI)

- Suruali mbili (2) au zaidi za light blue/bluu bahari kitambaa kizito.
- Shati mbili au zaidi nyeupe za mikono mirefu.
- Tai ndefu ya light blue/bluu bahari ya kitambaa kizito.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na kisigino kifupi.
- Soksi ndefu nyeupe.
- Mkanda mweusi wa ngozi wenye rungu ndogo.

NB: Unashauriwa kuja na pesa za kushonea sare za shule pamoja na sare ya kushindia shuleni ili kuepuka tatizo la kushona rangi isiyotakiwa na mtindo usiyotakiwa. Shule itafanya utaratibu wa kuleta fundi wa kushona nguo hapa Shuleni kwa sababu wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya Shule.

B. SARE YA SHULE (KUSHINDIA)

- T-shirt 2 za njano zenye nembo ya shule.
- Suruali 2 au zaidi za rangi ya kaki
- Nguo za michezo (Bukta na T-shirt za bluu).
- Sweta lililofumwa la rangi nyeusi kwa wenye uhitaji.
- Shuka mbili light blue/ bluu bahari.

NB: Unashauriwa kuja na pesa za kununua ili kuepuka kununua nguo za rangi zisizotakiwa.

C. MAHITAJI MENGINE MUHIMU

- Pia unapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:-
 - Fyekeo moja
 - Mfagio laini wa ndani (soft bloom).
 - Mfagio mgumu wa kusafishia sakafu (hard bloom).
 - Mopa moja.
 - Jembe likiwa kwenye mpini.

Mahitaji haya yatagawanywa katika mikondo ili kuepuka mwanafunzi mmoja kuwa na mzigo mkubwa

- Rimu mbili za karatasi za photocopy A4 kwa ajili ya mazoezi na mitihani kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni (F V & F VI)
- Ndoo kubwa ya lita 20
- Godoro la futi 2.5 .
- Picha ndogo 3 (passport size)
- Tsh.5,000/= kwa ajili ya Kitambulisho. (Njoo nazo mkononi Shuleni)
- Fomu ya hospitali (FORM FOR MEDICAL EXAMINATION) ambayo imeambatishwa katika barua hii. Ijazwe na daktari katika hospitali ya serikali na kugongwa muhuri.
- Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi iliyojazwa kwa usahihi ambayo imeambatishwa kwenye barua hii.
- Kivuli cha nakala halisi ya cheti cha kuzaliwa.
- Pesa ya Bima ya Afya Sh. 2,000/= (Njoo nazo mkononi Shuleni)

ANGALIZO:

- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani, mwanafunzi atakayekaidi agizo hili atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.
- Mwanafunzi asome kwa makini sheria za shule zilizoambatishwa kwenye barua hii na azizingatie.
- Mwanafunzi afikapo Shuleni, hataruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya Shule bila ruhusa ya maandishi toka kwa Mkuu wa Shule.

D. KARO

Karo ya shule kwa mwaka ni Tsh. 70,000/=. Mwanafunzi anatakiwa kulipa Tsh. 35,000/= kwa muhula au 70,000/= kwa mwaka.

E. MICHANGO MINGINE

- Tahadhari..... 5,000/=
- Taaluma 10,000/=
- Ulinzi..... 5,000/=
- Kiti na meza..... 15,000/=

NB: Malipo yote katika kipengele D na E yafanyike Benki katika Tawi lolote la **NMB** na siyo Shuleni. Akaunti ya Shule ni Na. **31501100460** , Jina la akaunti ya Shule ni **NGUDU SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION ACCOUNT**. Njoo na stakabadhi ya malipo shuleni.

F. MAHITAJI YA DARASANI

- Vitabu vya kiada na ziada kulingana na mchepuo wa mwanafunzi.
- Scientific calculator(Non Programmable) na Mathematical set kwa wanafunzi wa mchepuo wa sayansi, HGL na HGK
- Kalamu za wino, penseli na mfuto .

KUMBUKA:

Masomo yataanza rasmi siku ya Jumatatu tarehe 11/07/2016.

KUSOMA NI HAKI YA MSINGI YA MWANAO ITAKAYOMUONDOA KWENYE UJINGA, MARADHI NA UMASIKINI KWANI ELIMU NI RASILIMALI ISIOCHUJA.

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA. KARIBU SANA NGUDU



**J. C. KIMASA
MKUU WA SHULE**



MAWASILIANO: 0754310061
0713761378

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978.

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;-

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la msingi.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
- (d) Kuwahi katika shughuli za shule na zingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- 1. Wizi
- 2. Uasherati na ushoga
- 3. Ubakaji
- 4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, kubeli n.k
- 5. Kupigana au kupiga
- 6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- 7. Kudharau Bendera ya Taifa.
- 8. Kuoa au kuolewa
- 9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
- 10. Kutoa mimba
- 11. Kugoma, kuchohchea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- 12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
- 13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

**KWIMBA DISTRICT COUNCIL
NGUDU SECONDARY SCHOOL
FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

(To be completed by the Medical Officer in respect of all form five students)

PUPIL'S FULL NAME:.....

AGE:..... YEAR..... SEX.....

STOOL EXAMINATION.....

BLOOD COUNT (RED AND WHITE):.....

URINALYSIS:.....

SYPHILYSIS TEST:.....

T.B. TEST:.....

CHEST:.....

SPLEEN:.....

ABNORMAL INFORMATION e.g. Physical defects, impairment, chronic or family diseases etc.

.....
.....
.....
.....

I certify that I have examined the above student and recommend that He/ She is fit/unfit to pursue further education.

Signed

Designation

Date Official stamp.....

(Delete whichever is inapplicable)

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA
SHULE YA SEKONDARI NGUDU
MAELEKEZO KUHUSU HISTORIA NA MAKAZI YA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI

A. MAELEZO BINAFSI

1. Jina la Mwanafunzi.....kidato.....Jinsia (ME/KE).
2. Kabila.....Dini.....Tarehe ya kuzaliwa.....
3. Uraia

B. WAZAZI/ WALEZI

1. Jina la baba..... Je, Yupo hai (NDIYO/ HAPANA)
2. Jina la mama..... Je, Yupo hai (NDIYO/ HAPANA)
3. Kama baba na mama wamefariki/ wanaishi mbali;
 - i. Jina la mlezi wako ni.....Uhusiano wako na mlezi ni (Mjomba, Shangazi, baba mdogo, n.k).....
 - ii. Kazi ya baba/mlezi..... Eneo la Kazi/Idara.....
 - iii. Kazi ya mama.....Eneo la kazi/Idara.....

Wazazi wako wanaishi pamoja au wametengana ?

C. MAKAZI YA WAZAZI/ WALEZI

Wazazi wangu wanaishi;

- i. Baba wilaya.....kitongoji.....
Mtaa namba ya nyumba.....
- ii. Mama wilaya.....kitongoji.....
Mtaa namba ya nyumba.....
Simu.....Baba/mama/ mlezi.

D. MAKAZI YA MWANAFUNZI

- i. Je, wewe (Mwanafunzi) unaishi wapi ?
- ii. Je, unaishi na wazazi wako? (NDIYO/HAPANA).Kama jibu ni Hapana, eleza unaishi kwa nani
Jina uhusiano.....
Mtaa namba ya nyumba.....
Kitongoji jina la mwenyekiti wa kitongoji.....
Umbali kutoka shuleni..... km. Unatumia muda gani kufika shuleni.....

E. MALENGO YAKO (VISION / MISSION)

VISION:Maishani mwangu nalenga kuwa (Dr, Mwalimu, Mwanasheria, n.k)

.....

F. TAMKO (DECLARATION)

Maelezo niliyotoa hapo juu ni sahihi,

Jina..... saini..... Tarehe.....